TARGETER WINGS

KUTATHMINI HATUA YA MWANAFUNZI

Wings 001

GREDI 5 - 2024

SHUGHULI ZA KISWAHILI

Muda: Saa 1

KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

Swali la 1 hadi la 5.

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

(Ni siku ya kwanza shuleni baada ya likizo ya Disemba. Suna wanakutana na Moni wakielekea shuleni)



Suna : Hujambo moni?

Moni : *(akimnyoshea mkono)* Sijambo Suna. Habari za likizo?

Suna : Njema labda wewe. Likizo ilikuwaje?

Moni : *(Kwa furaha)* Lo! Nakuambia dadangu likizo yangu ilikuwa na shughuli tele na ziara si haba, sijapata kutulia hata ng'o! Si harusi, si matanga shughuli zilinibana.

Suna : *(Kwa mshangao)* Vipi tena?

Moni : *(Akitabasamu)* Ah! Usijali rafiki yangu. Nilizuru ughaibuni kumjulia hali dada yangu. Safari nyingine zilikuwa za humu humu tu. Namshukuru Mungu likizo imekamilika vizuri na tumerudi shule tukiwa wazima wa afya. Je, wewe.....

Suna : Hmmh ..... likizo yangu haikuwa na chochote cha maana. Sikusafiri popote kwani mama yangu hakupata nafasi. Naye nyanya hajapata nafuu.

Moni : *(Kwa masikitiko)* Oh! Maskini wamaanisha nyanya bado hajapata afueni baada ya upasuaji? Mola ampe neema zake.

Suna : Hata hivyo hatujakata tamaa tuna imani atapona na kurejelea shughuli zake.

Moni : Pole rafiki yangu. Namwombea afueni ya haraka. Nitakuja kumjulia hali kwa mara nyingine.

1. Likizo ya Moni ilikuwa ya
   A. ziara na sherehe
   B. sherehe na kazi nyingi
   C. ziara, sherehe na shughuli nyinginezo
   D. kazi nyingi na ziara
2. Ughaibuni ni
   A. miji ya mbali
   B. nchi za mbali
   C. kwenye starehe nyingi
   D. miji mikubwa mikubwa
3. Likizo ya Suna na Moni ilitofautiana namna gani?
   A. Mmoja hakuwa na shughuli kama mwenzake
   B. Mmoja alifurahia ilhali mwenzake hakufurahia.
   C. Mmoja alikuwa na starehe kuliko likizo za awali.
   D. Mmoja alisafiri ilhali mwingine hakusafiri.
4. Chagua jawabu sahihi kulingana na mazungumzo.
   A. Moni hakujua kuwa nyanyaye Suna alikuwa mgonjwa.
   B. Suna na Moni hawajawahi kushughulikia wagonjwa.
   C. Moni alitanya mambo mengi likizoni.
   D. Mazungumzo haya yanafanyika shuleni.
5. Moni anajali hali za watu wengine. Chagua kauli inayothibitisha ukweli huu
   A. Anapenda kuwatembelea wagonjwa.
   B. Anapenda kuzuru maeneo mbalimbali.
   C. Anamcha Mungu.
   D. Ana uhusiano mwema na dada yake.